Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Septemba

TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.10 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz

HALIUZWI

Bima ya Kilimo ni Mkombozi kwa Wajasiriamali

Yaliyomo

02

01 TIRA yatoa Semina ya Elimu ya Sheria ya Bima kwa Mahakimu jijini Dar es Salaam

02 Wahanga wa Ajali ya Moto Soko la Mashine Tatu Iringa Wafidiwa na Bima

04 TIRA Yashiriki Matembezi Kuadhimisha Siku ya Wagonjwa wa Sickle Cell Arusha

05 TIRA yashiriki Maonesho ya 8 ya Teknolojia ya Madini Geita, Elimu ya Bima Yatolewa

07 TIRA, NMB Kuhakikisha Bima Inamfikia kila Mtanzania

08 TIRA na Wadau wa Bima Watoa Msaada 8 Shule ya Sekondari Jangwani

08 TIRA yawanoa Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Tabora

11 TIRA Yaunga Mkono Ubunifu na Ushirikiano katika Soko kwenye Mkutano wa TIBA Zanzibar

12 TIRA yatoa Semina ya Elimu ya Sheria ya Bima kwa Mahakimu Mkoa wa Singida

Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma

Mhariri
Hadija Maulid

Waandishi
Tabia Mchakama
Anna Massao

Msanifu
Abubakari W. Kafumba

TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRA Updates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Septemba 2025.

Scan
Kusoma Kidijiti

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
info@tira.go.tz

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
www.tira.go.tz

TIRA yatoa Semina ya Elimu ya Sheria ya Bima kwa Mahakimu jijini Dar es Salaam

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeendendesha semina ya elimu ya Sheria ya Bima kwa Mahakimu Wakazi wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya wa Mkoa wa Dar es Salaam tarehe 12 Septemba 2025 kwa lengo la kuwajengea uelewa mpana kuhusu masuala ya bima na kuongeza ufanisi katika kushughulikia mashauri yanayohusiana na sekta hiyo.

Katika wasilisho lake Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware alieleza kuwa; Uhusiano kati ya Mahakama na TIRA umejengwa kwa kutumia msingi wa Sheria ya Bima Sura 394. Pamoja na majukumu mengine, TIRA na Mahakama wanalojukumu la Kulinda haki ya mkata bima (Mwananchi) na haki ya mkatisha bima (mwekezaji).

Zaidi alibainisha kuwa takwimu zilizopo TIRA zinaonyesha kwamba asilimia 95% ya madai ya waathirika hulipwa kila mwaka na kampuni za bima; hata hivyo ni asilimia 5% tu ya madai yanachukua muda mrefu kwa ajili ya kuhakikiwa na kujiridhisha na pia hupelekwa TIRA, Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) na Mahakamani kwa ajili ya usuhulishi na kupata haki.

Semina hiyo pia ilitoa fursa ya kipindi cha majadiliano ambapo maswali mbalimbali yaliulizwa na kujibiwa ipasavyo na Maafisa kutoka Mamlaka.

Wahanga wa Ajali ya Moto Soko la Mashine Tatu Iringa Wafidiwa na Bima

Wahanga wa ajali ya moto katika Soko la Mashine Tatu mkoani Iringa wamefidiwa kiasi cha shilingi milioni 120 na Kampuni ya Bima ya Reliance Septemba 18, 2025. Fidia hiyo imelipwa kufuatia tukio la moto lililotokea tarehe 12 Julai, 2025 na kuteketeza soko hilo kwa kiasi kikubwa.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi hundi ya fidia kwa wahanga hao, Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware, alitoa pole kwa wahanga na kusisitiza kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) itaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kampuni zote za bima nchini zinatekeleza majukumu yao kwa uaminifu, ufanisi na kwa wakati ili kuleta manufaa kwa wanufaika wa huduma za bima.

Dkt. Saqware pia alitoa rai kwa watoa huduma wote wa bima kuhakikisha kuwa madai ya wateja yanalipwa kwa wakati na kwa usahihi ili kuimarisha imani ya wananchi juu ya sekta ya bima hapa nchini.

Aidha, aliipongeza kampuni ya bima Reliance na Benki ya NMB kwa kushirikiana kutoa fidia kwa wahanga kwa haraka na kwa uwazi.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Reliance, Bw. Ravi Shankar, alisema kuwa kampuni yake imetimiza wajibu wake kwa kuwafidia wahanga hao kama sehemu ya dhamira ya Reliance Insurance ya

kuwakinga Watanzania wanapopatwa na majanga.

Alisema, "Baada ya tukio la moto katika Soko la Mashine Tatu, tulichukua hatua za haraka kwa kushirikiana na Benki ya NMB kufika moja kwa moja eneo la tukio. Tuliona ni vyema tuwafikie wateja wetu badala ya kuwasubiri waje ofisini kudai fidia. Tulikusanya taarifa zote muhimu kwa haraka na kuanza mchakato wa malipo. Hatua hii imeendelea kujenga imani na kuonesha kuwa soko la bima ni salama na linalojali walaji."

Naye Mkuu wa Idara ya Bima kutoka Benki ya NMB, Bw. Martine Massawe, alisema kuwa fidia waliyopewa wafanyabiashara hao 40 itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza makali ya hasara waliyoipata kutokana na janga hilo, na hivyo kuwawezesha kurejea katika shughuli zao za kiuchumi kwa haraka. Alisema, "NMB inatoa huduma za bima kwa wafanyabiashara wadogo kuanzia bima ya shilingi elfu kumi hadi laki tano. Kupitia huduma hizi, mfanyabiashara anaweza kupata fidia ya hadi milioni kumi kutegemeana na kiwango cha bima alichokichukua.

Tumeweka viwango vinavyolingana na uwezo wa wafanyabiashara ili kila mmoja apate fursa ya kujilinda dhidi ya majanga. Pia, NMB imeboresha mifumo ya kushughulikia madai kwa haraka ili wahusika waweze kurejea kwenye shughuli zao bila kuchelewa."

Bw. Massawe aliongeza kuwa licha ya fidia waliyopewa, wahanga hao bado wana uwezo wa kupata mikopo ya kuendeleza na kukuza biashara zao kupitia huduma za kifedha zinazotolewa na NMB.

TIRA Yashiriki Matembezi Kuadhimisha Siku ya Wagonjwa wa Sickle Cell Arusha

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia Kanda ya Kaskazini, tarehe 10 Septemba 2025 ilishiriki matembezi maalum ya kuadhimisha Siku ya Wagonjwa wa Sickle Cell yaliyofanyika jijini Arusha, katika Hospitali ya Mount Meru.

Katika maadhimisho hayo, Afisa Bima wa TIRA Kanda ya Kaskazini, Bw. Goodluck Massawe, alipata fursa ya kutoa elimu kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya. Alisisitiza kuwa bima ya afya ni nyenzo muhimu inayoweza kuwasaidia wananchi kuepuka gharama kubwa za matibabu, pamoja na kuhakikisha wanapata huduma bora na za uhakika.

Aidha, Bw. Massawe alieleza kuwa TIRA kwa sasa imeanza kusajili vituo vya afya vitakavyoshiriki katika mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote, kama sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote iliyopitishwa hivi karibuni.

Alibainisha kuwa hatua hiyo inalenga kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za afya kwa urahisi na kwa gharama nafuu. Vilevile, TIRA ilitumia fursa hiyo kuufahamisha umma kuwa Hospitali ya Mount Meru tayari imesajiliwa rasmi na Mamlaka, hatua inayowezesha kituo hicho kutoa huduma chini ya mfumo wa bima ya afya. Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya afya, watoa huduma na wananchi, ambapo pamoja na matembezi, washiriki walipata elimu kuhusu namna bora ya kujikinga na kudhibiti ugonjwa wa Sickle Cell.

TIRA yashiriki Maonesho ya 8 ya Teknolojia ya Madini Geita, Elimu ya Bima Yatolewa

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia Kanda ya Ziwa imeshiriki katika Maonesho ya Nane (8) ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika kwenye viwanja vya Dkt. Samia Suluhu Hassan, mkoani Geita kuanzia Septemba 22 – 28, 2025.

Katika maonesho hayo, kampuni mbalimbali za bima zilishiriki ndani ya banda moja maarufu kama "Kijiji cha Bima", ambapo zilitoa elimu na huduma za bima kwa wananchi waliotembelea mabanda hayo pamoja na wafanyabiashara na wafanyakazi wa migodini. Lengo kuu likiwa ni kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa bima katika kujikinga dhidi ya ajali na hatari mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika shughuli za kila siku.

Kaimu Meneja wa TIRA Kanda ya Ziwa Bw. Oyuke Phostine alieleza lengo la ushiriki huo ni kuweka thamani katika mnyororo wa shughuli za madini nchini Tanzania kwa kuelimisha wafanyakazi, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla umuhimu wa kujikinga na bima katika kazi zao mathalani kuwa na bima za afya.

Maonesho ya Teknolojia ya Madini yalianzishwa mwaka 2018 kwa lengo la kuimarisha sekta ya madini nchini na kuhakikisha rasilimali hiyo muhimu inanufaisha Watanzania wote. Maonesho hayo yamekuwa jukwaa mahsusi la Serikali, sekta binafsi, wachimbaji wakubwa na wadogo, taasisi za kifedha, wajasiriamali na wadau wa maendeleo kukutana, kujadili na kubadilishana uzoefu.

Maonesho hayo yaliongozwa na kauli mbiu "Ukuaji wa Sekta ya Madini ni Matokeo ya Matumizi ya Teknolojia Sahihi na Uongozi Bora Shiriki Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2025."

KIJIJI CHA BIMA
MAONESHO YA NANE YA KITAIFA YA TEKNOLOJIA YA MADINI 2025-GEITA
"Ukuaji wa Sekta ya Madini ni matokeo ya Matumizi ya Teknolojia Sahihi na Uongozi Bora, Shiriki Uchaguzi Mkuu 2025"
KIJIJI CHA BIMA
MAONESHO YA NANE YA KITAIFA YA TEKNOLOJIA YA MADINI 2025-GEITA
MUA
Britam
Newtan INSURANCE
ZIC
KARIBU

TIRA, NMB Kuhakikisha Bima Inamfikia kila Mtanzania

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Septemba 11, 2025 ilifanya kikao cha mashirikiano na wanahisa wa benki ya NMB kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya benki hiyo na sekta ya bima nchini.

Kupitia kikao hicho, TIRA na NMB wamekubaliana kuweka mikakati endelevu itakayowezesha kila Mtanzania kufikiwa na huduma za bima kupitia mifumo na mitandao ya kibenki.

Aidha, pande hizo mbili zilijadili namna benki zinavyoweza kuchangia katika kukuza sekta ya bima nchini, hususan katika eneo la bima za kilimo, pamoja na kushirikiana katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

TIRA na Wadau wa Bima Watoa Msaada Shule ya Sekondari Jangwani

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya bima wametoa msaada wa fanicha za kisasa kwa wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Jangwani tarehe 22 Septemba,2025, ikiwa ni sehemu ya juhudi za sekta hiyo katika kurudisha kwa jamii kupitia mpango wa Uwajibikaji wa Kijamii (CSR).

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano, Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware alisema sekta ya bima imetoa viti 200 na meza 200 kwa wanafunzi, pamoja na viti 32 na meza 32 kwa walimu. Msaada huo umelenga kupunguza uhaba wa samani unaoikabili shule hiyo yenye idadi kubwa ya wanafunzi.

"Mazingira bora ya kujifunzia ni nguzo muhimu ya mafanikio ya kitaaluma kwa wanafunzi. TIRA itaendelea kushirikiana na wadau wa elimu kuhakikisha elimu bora inapatikana kwa wote," alisema Dkt. Saqware.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Jangwani Bi. Nyaibuli Bhoke alitoa shukrani kwa sekta ya bima kwa msaada huo, akieleza kuwa utasaidia kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji shuleni hapo. Wanafunzi wa shule hiyo nao hawakuficha furaha yao,kupitia ujumbe wa shukrani uliosomwa na Dada Mkuu wa Shule hiyo, Bi. Neema Evance, mwanafunzi wa Kidato cha Sita (CBN), walisema msaada huo umewapa hamasa ya kujifunza kwa bidii, huku wakibainisha kuwa uwepo wa madawati na viti vya kutosha utapunguza msongamano na kuboresha mazingira ya kujifunza, hasa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Miongoni mwa kampuni za bima zilizoshiriki katika msaada huo ni pamoja na TAN-RE, GRAND-RE, na kampuni ya bima ya MO.

TIRA yawanoa Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Tabora

Tarehe 15 Septemba 2025; Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia Kanda ya Tabora ilifanya Mkutano na Waandishi wa Habari wa Mkoa huo (TABORA PRESS CLUB) kwa lengo la kutoa elimu kwa waandishi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya bima nchini na Mamlaka kwa ujumla hususan kuhusu majukumu ya Mamlaka, mchakato wa usajili wa watoa huduma za bima, namna ya kushughulikia malalamiko ya wateja na mifumo ya kidigitali inayotumika na Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake.

Wakati wa Hotuba yake Bi. Awanje Matenda, Meneja wa TIRA Kanda ya Magharibi alisema Mamlaka ina wajibu wa kusimamia, kudhibiti na kuendeleza sekta ya bima nchini Tanzania. Majukumu mengine ni pamoja na Kutoa leseni na kuhakikisha watoa huduma za bima wanazingatia sheria, kanuni na taratibu, kutoa elimu ya bima kwa umma kuhusu umuhimu wa bima, Kulinda maslahi ya bima na walaji wake lakini pia Kuishauri Serikali kuhusiana na Masuala ya Bima. "Waandishi wa Habari ni Daraja kati ya TIRA, Wadau wa Bima na Wananchi, hivyo tunaomba mkaandike taarifa za kweli na za uhakika kuhusu masuala ya bima kwani hili ni suala mtambuka linalotakiwa kujulikana na jamii ili majanga mengi yaweze kukingwa na kufidiwa" alisisitiza Meneja Awanje.

Naye, Afisa Bima Bi. Lea Mwakanosya kutoka Kanda hiyo, alieleza namna ya kusajili kampuni au wakala na huduma nyingine za bima nchini na kueleza baadhi ya vigezo na masharti ya kufuata

ambapo kikubwa ni kusajiliwa rasmi na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania. Baadhi ya vigezo vingine ni pamoja na kuwa na mtaji unaokidhi vigezo vya kisheria, kuwa na miundombinu na rasilimali watu inayofaa, kuwasilisha nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na mpango wa biashara, taarifa za kifedha, na cheti cha usajili kutoka BRELA, kupitia mchakato wa uchambuzi wa maombi na vibali kutolewa kwa waliokidhi masharti.

Mafunzo hayo yalihitimishwa na Bwn. Paul Nicholaus, Afisa TEHAMA wa Mamlaka kwa kuelimisha juu ya mifumo ya kidigitali inayoboresha utoaji huduma na usimamizi wa sekta ya bima kwa ujumla.

Miongoni mwa Mifumo aliyoielezea Afisa huyo ni pamoja na Mfumo wa TIRAMIS - Mfumo wa usimamizi wa taarifa za bima unaowezesha kampuni kuwasilisha taarifa kwa njia ya mtandao na ndio unaowapa polisi na raia taarifa za uhai wa bima kwenye vyombo vya moto.

Nao Waandishi wa habari walipata nafasi ya kuuliza maswali na kujadili changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika sekta ya bima nchini, hasa maeneo ya uelewa mdogo wa wananchi na ucheleweshaji wa fidia.

Mamlaka iliahidi kuendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa bima na haki za walaji na kwamba mikutano ya aina hiyo itaendelea kufanyika mara kwa mara.

TIRA Yaunga Mkono Ubunifu na Ushirikiano katika Soko kwenye Mkutano wa TIBA Zanzibar

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeshiriki katika Mkutano wa Umoja wa Madalali wa Bima Tanzania (TIBA) uliofanyika katika hoteli ya Golden Tulip visiwani Zanzibar kuanzia tarehe 24 -26 Septemba ambapo Septemba 26, 2025 ambapo ulifunguliwa rasmi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhandisi Zena A. Said. Katika mkutano huo Mamlaka iliongoza Mjadala unaohusu Usimamizi (Regulation), Ubunifu (Innovation), na Ushirikiano (Collaboration) kwa lengo la kukuza sekta ya bima ili kuongeza ufanisi, utoaji huduma jumuishi na kulinda maslahi ya wananchi.

Wadau katika sekta waliohudhuria Mkutano huo walipata nafasi ya kujadili kwa kina kuhusu juhudi zinazofanywa na Mamlaka kutatua changamoto mbalimbali, ikiwemo athari za maendeleo ya teknolojia kama matumizi ya Akili Mnemba (AI).
Katika maelezo yake, TIRA ilisisitiza dhamira yake ya kuhakikisha soko la bima linabaki salama kwa wadau na wateja kwa kushiriki mara kwa mikutano na wadau katika sekta ya bima wakiwemo TIBA ambapo kupitia mikutano hiyo na majukwaa tofauti shirikishi Mamlaka inapata sauti za wadau moja kwa moja na hatimaye kupata masuluhisho ya maswala mbalimbali yenye kuzingatia hali halisi ya sekta.

Mamlaka pia ilieleza kuhusu maboresho ya mifumo ya kidijitali inayolenga kupunguza urasimu, kuongeza uwazi, na kurahisisha ufuatiliaji wa madai pamoja na huduma za bima kwa ujumla.

Mjadala huo muhimu katika Sekta ya Bima ulishirikisha viongozi mbalimbali katika sekta akiwemo Bi. Magreth Mngumi, Msuluhishi wa Migogoro ya Bima ambaye alimuwakilisha Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware.

Majadiliano hayo yalikuwa matokeo ya Mkutano wa siku mbili uliofanyika visiwani hapo ambapo ulifunguliwa rasmi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhe. Mhandisi Zena A. Said.

TIRA yatoa Semina ya Elimu ya Sheria ya Bima kwa Mahakimu Mkoa wa Singida

Tarehe 26, Septemba 2025 – Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) – Kanda ya Magharibi iliendesha semina ya elimu ya Sheria ya Bima kwa Mahakimu Wakazi wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya za Mkoa wa Singida katika ukumbi wa Jmax, Wilaya ya Manyoni.

Lengo kuu la semina hiyo lilikuwa kuwajengea Mahakimu uelewa mazuri zaidi kuhusu masuala ya bima, ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia mashauri yanayohusiana na sekta ya bima. Kupitia semina hiyo, TIRA imeendelea kuimarisha ushirikiano na mhimili wa Mahakama, kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sheria za bima unafanyika kwa ufanisi, uwazi na kwa manufaa ya wananchi.

Meneja wa Kanda ya Magharibi Bi Awanje Matenda alisisitiza dhamira ya TIRA kuendelea kutoa elimu na kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya bima ili kuhakikisha kuwa haki na wajibu wa wadau wote wa bima unazingatiwa na kulindwa ipasavyo.

Semina hiyo pia iliwahusisha Wanasheria kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima ambao walitoa somo kuhusu Sheria hizo kufatwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Bima ni nini?

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina

ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa

kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za uJulainga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.

TIRA & 2025

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

FB, IG, X: //@tira_tz
www.tira.go.tz